TALKING NOTES ZA KATIBU MKUU WIZARA YA MADINI KATIKA HAFLA YA UNUNUZI WA MADINI YA TANZANITE ITAKAYOFANYIKA TAREHE 27 AGOSTI, 2022 KATIKA ENEO LA MIRERANI – SIMANJIRO, MANYARA

Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Waziri wa Madini;

Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri wa Fedha na Mipango;

Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb.), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi;

Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax (Mb.), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;

IGP. Camillus Mongoso Wambura, Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania;

CP. Salum Hamduni, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU);

Jenerali Jacob Mkunda, Mkuu wa Majeshi (CDF);

Mhe. Charles Makongoro Nyerere, Mkuu wa Mkoa wa Manyara;

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa Mliopo;

Mhe. Dkt. Stephen Lemono Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini;

Ndugu Emmanuel Mpawe Tutuba, Katibu Mkuu – Wizara ya Fedha na Mipango;

Dkt. Faraji K. Mnyepe, Katibu Mkuu – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT);

Prof. Riziki Silas Shemdoe, Katibu Mkuu – TAMISEMI;

Dkt. Allan Kijazi, Katibu Mkuu – Wizara ya Ardhi;

Dkt. Evaristo Longopa, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Prof. Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu;

Bi. Karolina Albert Mthapula, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara;

Makatibu Tawala wa Mikoa Mliopo;

Ndugu Msafiri Mbibo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini;

Mhe. Dkt. Suleiman Selela, Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro;

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya Mliopo;

Mhe. Dustan Kitandula (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini;

Mhe. Christopher Ole Sendeka (Mb.), Mbunge wa Wilaya ya Simanjiro;

Viongozi wa CCM Mkoa wa Manyara na Wilaya ya Simanjiro;

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Simanjiro;

Dkt. Abdulrahman S. Mwanga, Kamishna wa Madini;

Prof. Idris Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini;

Mhandisi Yahya Samamba, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini;

Dkt. Venance Mwase, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO);

Dkt. Mussa Daniel Budeba, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST);

Bi. Mariam Mgaya, Kaimu Mtendaji Mkuu wa TEITI;

Ndugu Daniel Kidesheni, Kaimu Mratibu wa Chuo cha Jemolojia Tanzania (TGC);

Watendaji wa Wizara ya Madini;

Watendaji wa Tume ya Madini;

Watendaji mbalimbali wa Serikali;

Ndugu John Bina, Rais wa FEMATA;

Ndugu Haroun Kinega, Katibu Mtendaji wa FEMATA;

Ndugu Samuel Mollel, Katibu wa TAMIDA;

Viongozi wa Mkoa wa Vyama ya Wachimbaji wadogo na Wafanyabiashara ya Madini;

Wachimbaji na Wafanyabiashara wakubwa wa madini (Ndg. Saniniu Laizer, Bw. Anselim Kawishe, Franone Mining n.k);

Viongozi wa Dini Wilaya ya Simanjiro;

Wananchi wa eneo la Mirerani;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana!

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Waziri, Awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuweza kutukutanisha mahali hapa siku ya leo, tukiwa na afya njema kwa ajili ya kushuhudia ununuzi wa vipande vya madini ya tanzanite yenye sifa za kipekee ambavyo vimezalishwa katika mgodi wa mchimbaji mdogo, **Bw. Anselim J. Kawishe**.

Mheshimiwa Waziri, Kipekee, napenda nitumie nafasi hii kumshukuru **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuiwezesha Tume ya Madini ambayo ipo chini ya Wizara ya Madini kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa tija kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Mheshimiwa Waziri, Pamoja na shukrani zangu za dhati kwako, Viongozi wa Wizara, Prof. Idris S. Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini na Serikali kwa ujumla, naomba kukufahamisha kuwa, Tume ya Madini inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake kikamilifu kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123 ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yanayotokana na shughuli za madini, kupitia utoaji na usimamizi wa leseni za madini, kusimamia na kudhibiti uchimbaji, uchakataji na biashara ya madini nchini.

Mheshimiwa Waziri, Itakumbukwa kuwa, mwaka 2021/2022 Tume ya Madini ilikusanya shilingi bilioni **623.2** sawa na asilimia **95.8** ya lengo la kukusanya shilingi bilioni **650.** Kwa mwaka 2022/2023 Tume ya Madini imewekewa lengo la kukusanya shilingi bilioni **822** sawa na wastani wa shilingi bilioni **68.5** kwa mwezi. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 Tume ya Madini imekusanya jumla ya shilingi bilioni **57.6** sawa na asilimia **84.05** ya lengo kwa kipindi husika. Nakiri kuwa, madini ya tanzanite ni miongoni mwa madini yaliyochangia katika makusanyo hayo.

Mheshimiwa Waziri, Hadi kufikia tarehe 30 Julai, 2022 Tume ya Madini inasimamia leseni hai **95** za uchimbaji mdogo wa madini ya tanzanite na leseni **5** za uchimbaji wa madini ya tanzanite kati katika eneo la Mirerani. Kutokana na shughuli za uzalishaji zinazoendelea kufanyika katika leseni hizo katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 madini ya tanzanite ghafi kiasi cha **kilogramu 3,526.58** zenye thamani ya **shilingi 13,508,391,484.27** kilizalishwa. Mapato ya Serikali yaliyotokana tozo za madini katika uzalishaji huo ni jumla ya **shilingi 901,654,427.26** ambapo mrabaha ni kiasi cha **shilingi 770,444,539.39** na ada ya ukaguzi **shilingi 155,043,400.17**.

Mheshimiwa Waziri, Leo tutashuhudia ununuzi wa vipande viwili vyenye sifa ya kipekee vya madini ya tanzanite vilivyozalishwa katika leseni ya uchimbaji mdogo namba **PML002948NZ** inayomilikiwa na **Bw. Anselim J. Kawishe**. Thamani ya madini haya ilipatikana kutokana na vigezo vya kijemolojia ambavyo ni rangi *(color)*, ubora *(clarity)*, uzito *(carat weight)* na umbo *(cut/shape)* pamoja na muongozo wa bei elekezi ya Serikali. Kipande cha kwanza kina uzito wa **kilogramu 1.48,** rangi ya **AB (Uzuri wa Juu),** ubora wa **AB (Ubora wa Juu)** chenye thamani ya **shilingi 713,790,909.53** na kipande pili kina uzito wa **kilogramu 3.74**, rangi ya **BC (Uzuri wa Kati)**, ubora wa **BC (Ubora wa Kati)** chenye thamani ya **shilingi 1,531,780,633.93**. Jumla ya thamani ya madini hayo ni **shilingi 2,245,571,543.46.**

Mheshimiwa Waziri, Tume ya Madini inatoa pongezi kwa **Bw. Anselim J. Kawishe** kwa kufanikiwa kuzalisha madini hayo yenye thamani kubwa ambayo pamoja na kuchangia katika mapato ya Serikali, madini hayo pia yatatumika kuitangaza Tanzania Kimataifa na kuwa kivutio cha utalii kwa wageni na watanzania.

Mheshimiwa Waziri, Nitumie nafasi hii pia kutoa wito kwa wachimbaji wengine wadogo na wa kati kuendesha shughuli za uchimbaji kwa kufuata Sheria ya Madini, Sura ya 123 na Kanuni zake na kuepuka vitendo vya utoroshaji madini ili madini yanayozalishwa yaweze kulinufaisha taifa letu.

Mheshimiwa Waziri, Nashukuru sana kwa nafasi hii.